# UHAKIKI WA KAZI ZA FASIHI SIMULIZI

**Uhakiki ni nini?**

Ni kitendo cha kuchambua na kufafanua kazi ya fasihi kifani na kimaudhui ili kuweza kupata ujumbe uliomo katika kazi hiyo.

## Uhakiki wa ushairi wa fasihi simulizi

Ushairi ni fungu linalojumuisha tungo zote zenye kutumia mapigo kwa utaratibu maalumu. Mapigo hayo yanaweza kuwa na muwala wa urari wa vina na mizani.

### <u>Fani na Maudhui katika Ushairi</u>

Ushairi kama ilivyo kwa kazi nyingine za fasihi hujengwa kwa vipengele vikuu viwili (2) ambavo ni fani na maudhui.

### i) Fani katika ushairi

Katika ushairi wa fasihi simulizi, fani hujengwa kwa vipengele vifuatavyo:

- **Muundo**

Mashairi yana miundo mbalimbali kutokana na ufundi wa mshairi mwenyewe. Katika muundo huwa tunaangalia kile kinachoonekana kwa nje.

**Mfano:** - Mgawo wa vipande
- Idadi ya mistari katika kila ubeti
- Kiitikio, mkarara au kibwagizo
- Idadi ya beti katika shairi zima

Katika mashairi huwa kuna miundo mbalimbali ambayo hutumiwa kwa mujibu wa idadi ya mistari katika kila ubeti.

**Mfano:**

- ✓ **Tamolitha** - Ubeti wa shairi wenye mstari mmoja.
- ✓ **Tathnia** - Ni mashari yenye mistari miwili kwa kila ubeti.
- ✓ **Tathlitha** - Ni mashairi yaliyojengwa kwa mistari mitatu.
- ✓ **Tarbia** - Ni mashairi yaliyojengwa kwa mistari mine
- ✓ **Takhmisa** - Ni mashairi yaliyojengwa kwa mistari mitano.
- ✓ **Sabilia** - Ni mashairi yaliyojengwa kwa mistari mitano na kuendelea.
- ✓

- **Mtindo**

Mashairi ya fasihi simulizi huwa na mitindo mingi sana katika utungaji wake. Katika mtindo unachunguza vipengele vifuatavyo:

- ✓ **Mbinu ya uwasilishaji wa ujumbe**

Ni mbinu za kisanaa zinazotumiwa na msanii wa katika kutunga shairi lake. Mbinu hizo ni kama vile urari wa vina na mizani. (Ushairi wa kimapokeo)

- ✓ **Mtindo wa msisitizo**

Katika mtindo huu, neno moja hurudiwa rudiwa kila mstari. Mtindo wa msisitizo upo wa aina mbili, msisitizo wima na msisitizo mlalo.

- ✓ **Mtindo pindu**

Huu ni mtindo ambao silabi za mwisho za mstari hurudiwa rudiwa. Mfano: Mstari wa kwanza huishia na neno **inuka.** Mstari utakaofuata pia huanza na **inuka.**

**Hisia**

Kwa upande wa hisia, tunajiuliza maswali yafuatayo:
Ni hisia gani zinazowasilishwa na ushairi huru. Hisia hizo ni za kuogofya, furaha, kukata tama na kadhalika.

**Utendaji**

Katika utendaji, tunaangalia kama ushairi huo unatendwa na mtu mmoja , watu ama mtu mmoja akijibizana na kundi la watu wengi kwa zamu.

**Muktadha (mazingira) wa utendaji**

Hapa tunaangali kama ushairi:
- Umeimbwa wapi?
- Wakati gani?
- Kwa hadhira ya aina gani?
- Watendaji ni akina nani? Wazee, vijana wanaume au wanawake?
-

**Madoido/ Vichapuzi**

Madoido ni vitu ambavyo huambatana na sauti. Madoido ni kama vile makofi, vigeregere, kuruka kamba, manyanga na kadhalika.

**Wahusika**

Katika ushairi wa fasihi simulizi, kunakuwa na wahusika wa aina mbili ambao ni fanani na hadhira. Fanani hutumiwa na mtunzi katika kufikisha ujumbe wake kwa hadhira. Mfano, mwimbaji. Na hadhira ni wasikilizaji au watazamaji katika ushairi. Katika ushairi hadhira huweza kutokea kama waitikiaji.

**Matumizi ya lugha**

Lugha ndio malighafi ya ushairi. Lugha inaotumika ni ile lugha inayoibu hisia mbalimbali miongini mwa hadhira. Matumizi ya lugha katika ushairi ni ya aina mbalimbali:
- ***Uteuzi wa maneno au msamiati.***

Katika uteuzi wa maneno au msamiati, tunaangalia mambo yafuatayo:
- Matumizi ya maneno yaliyobuniwa na msanii mwenyewe.
- Matumizi ya tamathali za semi.
  Mfano; Tashbiha, sitiari na kadhalika
- Mbinu zingine za kisanaa.
  Mfano: Onomatopeia
- Matumizi ya mehali, misemo na naahau.
- Matumizi ya taswira na kadhalika

## Maudhui katika ushairi

Maudhui ni jumla ya mawazo yote yanayozungumzwa na mwandishi wa kazi ya fasihi. Maudhui hujumlisha mawazo pamoja na mafunzo mbalimbali yaliyomsukuma msanii hadi akatunga kazi Fulani ya kifasihi.

Tunapohakiki maudhui katika ushairi hwa tunaangalia vipengele vifuatavyo:

**(a) Dhamira:**

Ni kiini cha suala linalojadiliwa au linalozungumzwa katika ushairi. Katika ushairi huwa kuna dhamira kuu ambayo huwa ni lengo kuu lililomsukuma msanii wa kazi hiyo kutunga kazi yake na dhamira ndogondogo ambazo huenda sambamba na dhamira kuu. Wasanii wa fasihi hasa wa ushairi, huweza kushughulika na dhamira zifuatazo:

- *Mapenzi na ndoa*
- *Mwanamke na nafasi yake*
- *Ukombozi*
- *Maadili mbalimbali katika jamii na kadhalika.*

**(b) Ujumbe:**

Ujumbe katika kazi ya fasihi ni mafunzo mbalimbali ambayo hupatikana baada ya kusoma au kusikiliza ushairi wa fasihi. Katika kazi ya fasihi, ujumbe unaweza kuwa unatumia lugha ya kifasihi au usitumie lugha ya kifasihi.

**Mfano:**

- *Ili tuondokane na umaskini hatuna budi kufanya kazi kwa bidii.*
- *Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.*

**(c) Falsafa:**

Ni muelekeo wa imani ya mwandishi wa kazi ya fasihi. Falsafa ya msanii hujadili jinsi msanii wa kazi hiyo hasa wa ushairi anavyoamini katika kile anachokijadili.

**(d) Msimamo:**

Ni hali ya msanii kuamua kufuata na kulishikilia jambo fulani. Maranyingi, msimamo wa mwandishi hutegemea falsafa aliyonayo msanii wa kazi wa hiyo katika kulishikilia jambo hata kama halitakubalika na wengi.

**Swali:**

***Tunga wimbo wowote kisha fafanua kwa ufupi vipengele vya fani na maudhui vilivyotumikali katika wimbo huo.***